# Hatua Zinazofuata Baada ya Changamoto ya Biblia

www.thecenterforbiblicalstudies.org



Maelfu ya watu wameshashiriki kwenye Changamoto ya Biblia katika majimbo yote ya Marekani na ulimwenguni.  Washiriki wengi wamekiri kwamba kusoma Biblia limekuwa ni jambo muhimu la kiroho kuliko yote katika maisha yao.  Kumewawezesha kuona matendo makuu ya upendo wa Mungu katika historia na kuwafanya wajisikie kuwa karibu zaidi na Mungu kuliko wakati wowote.

Wengi wamesema, "Nilipenda Changamoto ya Biblia, lakini sasa nina maswali zaidi kuliko nilivyoanza." Hili ni jambo la kawaida.  Maswali yetu hututia moyo zaidi kuendelea kusoma na kujifunza zaidi.  Biblia ni maktaba yenye vitabu 66, na tunaweza daima kujifunza kwa kadri tunavyo imarisha imani yetu na kujenga tabia ya kiroho ya kusoma Neno la Mungu kila siku katika maisha yote.

John Adams, Rais wa pili wa Marekani, alisoma Biblia yote kila mwaka katika maisha yake ya utu uzima, akisoma Biblia ile ile tena na tena.  Tunaweza kuichakaza Biblia tunayoipenda sana na kuweka alama kwenye mistari inayotuvutia zaidi, kutuongoza na kututia nguvu.  Kwa wale wanaotamani kujaribu mambo mapya katika kujifunza kwao Biblia, tunawapa kuchagua njia zifuatazo:

## Ushauri kwa ajili ya Kujisomea Biblia Zaidi

**1. Jaribu kusoma Biblia katika tafsiri tofauti** – Baadha ya watu husoma Biblia katika tafsiri tofauti kila mwaka.  Kila tafsiri huweka maneno na vifungu kwa namna tofauti kidogo, hali ambayo huiwezesha Biblia kusema nasi kwa upya, kwa njia mpya.  Unaweza kuamua kuendelea kusoma sura tatu za Agano la Kale, zaburi moja na sura moja ya Agano Jipya kila siku au kupunguza kasi na kusoma sura moja tu ya Agano la Kale, zaburi moja na sura moja ya Agano Jipya kil siku.  Jambo la msingi ni kusoma kiasi fulani kila siku.

Tafsiri za Biblia zifuatazo zimeidhinishwa na Kanisa la Anglikana Marekani ili zitumike kwa usomaji wa Neno (Tunapendekeza mtumie zaidi matoleo ya Biblia tuliyoyaandikwa kwa wino mnene)

*Biblia ya King James au Authorized Version* (ni Bibli ya zamani zaidi katika Kanisa la Anglikana la Marekani, lakini ni ngumu zaidi kuisoma kuliko tafsiri nyingine).  Tembelea tovuti ya: www.thekjvstore.com
*Biblia ya English Revision* (1881)
*Biblia ya American Revision* (1901)
*Biblia ya Revised Standard Version* (1952)
*Biblia ya Jerusalem Bible* (1966)

***Biblia ya New English Bible yenye vitabu vya Apocrypha* (1970).** Tembelea tovuti ya: www.christianbook.com
*Biblia ya Good News Bible au Today's English Version* (1976) (toleo ambalo limetafsiriwa kwa kuifupisha Biblia)
***Biblia ya New American Bible* (1970).** Tembelea tovuti ya: www.amazon.com
***Biblia ya Revised Standard Version*, toleo la Umoja wa Makanisa.** Tembelea tovuti ya: www.amazon.com
***Biblia ya New International Version* (1978).** Tembelea tovuti ya: www.zondervan.com
***Biblia ya New Jerusalem Bible* (1987)** Tembelea tovuti ya: www.christianbook.com
***Biblia ya New Revised English Bible* (1989)** Tembelea tovuti ya: www.christianbook.com
***Biblia ya New Revised Standard Version* (1990)** Tembelea tovuti ya: www.nrsv.net
***Biblia ya Common English Version* (2011).** Tembelea tovutiya: www.commonenglishbible.com

**2. Soma Biblia kwa kutumia *Changamoto ya Biblia* –** Kitabu chetu cha *The Biible Challenge*, yaani Changamoto ya Biblia, kinaendana na mpango wa Soma Biblia kwa Mwaka pamoja na masoma yake ya kila siku yanayotumika ulimwenguni pote. Kitabu cha *The Bible Challenge*, yaani 'Changamoto ya Biblia' kinachapishwa na asasi ya *Forward Movement* na kinapatikana kwenye tovuti ya: http://www.forwardmovement.org/Products/2114/the-bible-challenge-read-the-bible-in-a-year.aspx au kwenye maduka ya *Amazon* au *Barnes and Nobles*.

**3. Mshirikishe mtu mwingine furaha yako ya kusoma Biblia –** kama umefurahia na kunufaika na usomaji wa Biblia kwa utaratibu wa kila siku, mshirikishe rafiki au mmoja wa familia yako kuhusu uzoefu ulioupata. Unaweza kuamua kumnunulia mmojawapo Biblia kama zawadi. Waambie kuhusu Changamoto ya Biblia, au uwaombe wakuruhusu ili uwaandikishe kuwa washiriki wa usomaji wa Biblia. Soma Biblia kwa mara nyingine pamoja nao na kutana nao mara kwa mara ili kuwashirikisha mawazo yako na uzoefu wako. Jambo hili litakuza uhusiano wenu na pia uhusiano na Mungu, na tena kila mmoja atajifunza toka kwa mwingine.

**4. Amua kusoma Biblia ukiwa na mtazamo maalum –** Wachapishaji siku hizi wanatoa matoleo mengi ya Biblia ambayo yanaonyesha kwa msomaji vifungu vyenye mtazamo maalum. Bibli hizo ni pamoja na:

Biblia iitwayo *The People's Bible*, yaani 'Biblia ya Watu' – Hii ni Biblia ya New International Version, yaani 'Toleo Jipya la Kimataifa', ambayo inatoa muongozo wa wazi wa vifungu vinavyosomwa zaidi na watu kwa kuvichapisha vifungu hivyo kwa maandishi makubwa yenye wino mnene. Tembelea tovuti hii: www.zondervan.com

Biblia iitwayo *The Peoples' Bible* yaani 'Biblia ya Watu' – ipo katika toleo jingine la *New Revised Standard Version*, yaani 'Toleo Sanifu lililopitiwa Upya', ambalo linaonyesha jinsi utamaduni ulivyotawala mtazamo wa Biblia na jinsi watu wanavyoisoma Biblia. Tembelea tovuti ya: www.augsburgfortress.com

Biblia iitwayo *The Jewish Annotated New Testament*, yaani 'Agano Jipya la Kiyahudi lenye Maelezo' – ipo katika toleo la Biblia la New Revised Standard Version, yaani 'Toleo Sanifu lililopitiwa Upya', ina maelezo ya kumsaidia msomaji kujifunza, yaliyoandikwa na jopo la kimataifa la wanazuoni wenye mtazamo wa Kiyahudi. Tembelea tovuti hii: www.oup.com au www.amazon.com

Biblia iitwayo *The Inclusive Bible*, yaani 'Biblia yenye lungha Isiyobagua' – Biblia hii yenye lugha isiyobagua [wanawake] inatupa tafsiri mpya ya Kiingereza yenye nguvu, na ambayo imesukwa kwa uangalifu ili kuonyesha nguvu na ushairi wa lugha ya Biblia. Tembelea tovuti ya: www.amazon.com

Biblia iitwayo *The Financial Stewardship Bible*, yaani 'Biblia ya Uwakili wa Fedha' – Biblia hii ya Kiingereza cha Kisasa inabainisha vifungu zaidi ya 2,000 vinavyohusu uaminifu, kipato, fedha na mali kwa ujumla. Tembelea tovuti hii: www.americanbible.org

Biblia iitwayo *The Poverty and Social Justice Bible*, yaani 'Biblia ya Umaskini na Haki' – Biblia hii inaonyesha vifungu ambavyo vinazungumzia utume, haki ya jamii, umaskini na kuwahudumia maskini na wahitaji. Tembelea tovuti hii: www.povertyandjusticebible.org

Biblia iitwayo *The Green Bible*, yaani 'Biblia ya Kijani' – Biblia hii ya *New Revised Standard Version*, yaani 'Toleo Sanifu lililopitiwa Upya', inatusaidia kuona maono ya Mungu kwa ajili ya uumbaji na jinsi tunavyoweza kufanya kazi ya kuhuisha na kuhifadhi mazingira. Tembelea tovuti hii: www.harpercollins.com

Biblia iitwayo *The Freedom Bible*, yaani 'Biblia ya Uhuru' – Biblia hii ipo katika toleo la Kiingereza cha Kisasa, na inaonyesha vifungu zaidi ya 3,500 ambavyo vinatufunulia ujumbe wa ajabu wa Biblia kuhusu uhuru. Tembelea tovuti hii www.americanbible.org

Biblia iitwayo *The Life Recovery Bible*, yaani 'Biblia ya Kurejesha Maisha' – hili ni toleo la *New Living Translation,* yaani 'Tafsiri ya Maisha Mapya', inawasaidia watu walioathirika na tabia zilizokithiri [zilizopita kiasi] waone chanzo kikuu cha uzima – Mungu mwenyewe. Tembelea tovuti hii: www.liferecoverybible.com

Biblia iitwayo *The C.S. Lewis Bible*, yaani 'Biblia ya C.S. Lewis' – Biblia hii ya *New Revised Standard Version*, yaani 'Toleo Sanifu lililopitiwa Upya', inaoanisha pamoja

nukuu toka kwa C.S. Lewis, mmoja wa waandishi walioheshimika sana katika Ukristo wa wakati huo. Tembelea tovuti hii: www.harpercollins.com

Biblia iitwayo *The Archeological Study Bible*, yaani 'Biblia ya Mtaala ya Mambo ya Kale' – Biblia hii ya *New International Version*, yaani 'Toleo Jipya la Kimataifa', inaonyesha mazingira ya Biblia ya mambo ya kale, historia na utamaduni, kadhalika uchimbaji wa mambo ya kale na ugunduzi ambao unatoa mwangaza kuhusu masimulizi ya Biblia. Tembelea tovuti hii: www.zondervan.com

**5. Soma Biblia kwa kutumia desturi ya zamani ya kimonaki iitwayo *lectio divina* –** Kwa karne kadhaa, wamonaki Wakristo wamesoma Biblia kwa mtindo wa polepole na wenye tafakari kwa kulithamini Neno la Mungu na kuliacha liseme nao kwa ndani kabisa. Desturi ya *Lectio divina* ina hatua nne: *lectio,meditatio, oratio* and *contemplatio* – yaani kusoma, kutafakari, kuomba, na kujifunza vifungu kwa kina. Chagua kitabu cha Biblia ili usome. Tunashauri uanze na injili mojawapo. Kwa wakati mmoja usisome zaidi ya sura moja, labda soma paragrafu moja au mbili kwa wakati mmoja.

Katika hatua ya kwanza, *lectio*, soma kifungu polepole. Unapoguswa na kitu, tulia kwa muda na tafakari neno hilo, msemo au mtari ambao umegusa hisia zako. Hatua hii ndiyo *meditatio*. Tafuta kifungu cha maandiko kama ng'ombe acheuwavyo majani. Kisha fanya maombi kwa Mungu kwa ufupi kuhusu kifungu husika na jinsi ambavyo Mungu amesema nawe. Hatua hii ndiyo *oratio*. Mwishowe, kaa kimya na kumsikiliza Mungu akisema nawe kimya kimya ndani ya moyo wako kwa kadri unavyomsubiri kwa faragha. Hatua hii ndiyo c*ontemplatio*. Hatu hii ya nne labda ndiyo muhimu kuliko zote na ni ngumu kuitenda katika desturi ya *lectio divina.*

Tembelea tovuti yetu ya: www.thecenterforbiblicalstudies.org na angalia chini ya kichwa kiitwacho *Maandiko* na utazame sehemu ya *Makala* ili kupata maelezo zaidi kuhusu desturi ya *lectio divina* au tembelea tovuti hii: www.lectio-divina.org Lengo la *lectio divina* ni kuleta mabadiliko ya kiroho na siyo mafunzo ya kitaaluma. Ni desturi inayofungua Neno la Mungu katiak njia ambazo wakati wote zinatuburudisha na kutuvutia.

**6. Kukariri maandiko –** Rich Warren, mwandishi wa kitabu kiitwacho *The PurposeDriven Life*, yaani 'Maisha Yenye Lengo' – kitabu ambacho kwa nyakati zote kimeuzwa kuliko vyote isipokuwa Biblia – anasema kwamba kukariri maandiko imekuwa ndiyo silaha muhimu ya kiroho kuliko silaha zote katika maisha na huduma yake. Tunapokariri kitu, kinakuwa sehemu ya maisha yetu. Tunaweza kukumbuka, kukisema upya na kukitumia kuumba mawazo yetu, kuongoza maamuzi yetu na kuyaeleza yale tunayoyaamini. Kuna tovuti yenye programu ya kompyuta iitwayo *BibleMinded* ambayo inakuwezesha kukariri mistari ya Biblia au kufuata kufuata mojawapo ya taratibu za usomaji wa Biblia zifuatazo.

Tunashauri usome sura moja ya Biblia kwa siku na kuwekea alama kifungu kimoja cha kukariri. Kiandike kifungu kwenye karatasi au kadi unayotumia kuwekea alama kwenye Biblia. Tumia dakika kadhaa ukijaribu kukariri hicho kifungu. Chukua karatasi hiyo uwe nayo, fanya mazoezi ya kurudiarudia kusema kifungu kwa siku nzima. Mwisho wa siku, utakuwa umeshakikariri kifungu husika. Vile vifungu uvipendavyo vipitiepitie aghalabu mara moja kwa wiki.

**7. Sikiliza Biblia** – Siku hizi kuna vifaa vingi vinavyoweza kukuwezesha kusikiliza Biblia unaposafiri kuelekea kazini, unapotembea na mbwa wako, unapofanya mazoezi, unaposafiri au ukiwa umepumzika nyumbani. Hili ni jambo jema sana kwa wale wenye kawaida ya kusikiliza zaidi kuliko kusoma na wale ambao hawawezi kusoma maandishi. Unaweze kusikiliza Biblia katika tafsiri mbalimbali kwa njia ya programu za kimtandao. Tembelea tovuti hizi: *www.Audio.com/Bible*, *www.listenersbible.com*, *www.BibleGateway.com*, *www.YouVersion.com* au *www.faithcomesthroughhearing.com*. Huduma iitwayo *Faith Comes through Hearing*, yaani 'Imani Huja kwa Kusikia', ina vifaa vizuri sana, ikiwemo kifaa cha kusikilizia cha MP3 ambacho kinakuwezesha kusikiliza Agano Jipya lote kwa njia ya sauti kwa kutumia dakika 28 kila siku kwa siku 40. Toleo la Biblia la *King James* na toleo la *New International Version* yanapatikana pia kwenye CD.

**8. Soma na Jifunze Injili Zinazofanana –** Injili ya Mathayo, Marko na Luka zina matukio yanayofanana. Wanafunzi wanaweza kusoma injili hizi katika ukurasa mmoja wenye jedwali na kulinganisha jinsi wainjilisti walivyoeleza mifano ileile, masimulizi au mafundisho. Unaweza kujifunza mwenyewe au katika kikundi.

Tunashauri utumie 1) *Gospel Parallels*, yaani 'Ulinganifu wa Injili', ni kitabu kilichohaririwa na Joel B. Green na W. Gil Shin wakitumia Biblia ya *Common English Bible*; 2) *Gospel Parallels*, yaani 'Ulinganifu wa Injili', ni kitabu kilichochapishwa na *Thomas Nelson Publishers,* yaani 'Wachapishaji wa Thomas Nelson', ambacho kinatumia toleo la Biblia la *Revised Standard Version*, yaani 'Toleo Sanifu Lililosahihishwa' au 3) kitabu cha *Records of the Life of Jesus*, yaani 'Kumbukumbu za Maisha ya Yesu', kinachotumia toleo la Biblia la *Revised Standard Version*, kilichoandaliwa na Henry Burton Sharman, na ambacho kinaweza kununuliwa kwenye duka la *Pendle Hill*. Tembelea tovuti hii: *www.pendlehill.org* Pia tunashauri kitachu kiitwacho *Approaching the Gospels Together cha* Mary C. Morrison, ambacho kinatoa mbinu mpya ya usomaji wa injili katika vikundi vidogo.

**9. Soma Apokrifa –** Apokrifa ni mkusanyiko wa vitabu vya zamani ambavyo vinapatikana katika tafsiri kuu kadha wa kadha za Biblia kama vile *New Revised Standard Version* ambazo hutumiwa na wa Protestanti na Wakatoliki. Apokrifa kwa kawaida katika Biblia hupatikana katika sehemu yake pake yake kati ya Agano la Kale na Agano Jipya au mwishoni mwa Agano Jipya. Vitabu vyote hivi, isipokuwa kitabu cha 2

cha Esdra, vilikuwemo katika tafsiri ya Kigiriki ya Agano la Kale iitwayo *Septuaginta* lakini havikuwa sehemu ya Agano la Kale la Kiebrania.

Neno "Apokrifa" linatokana na neno la Kigiriki lenye maana ya "mambo yaliyofichika", kwa kuwa maandiko haya yalifikiriwa kuwa yana mamboya mafumbo na hekima iliyofichika. Kanisa Katoliki, Kanisa la Kiothodoksi la Mashariki, Makanisa ya Kigiriki na Urusi yanaona kuwa vitabu hivi vina mamlaka, na vyafaa kwa mafundisho ya kweli ya imani na hivyo huviita *deutero-canon*, yaani 'kanuni ya pili [ya Maandiko]'. Waprotestanti huviita Apokrifa na hawaoni kuwa vyafaa kwa mafundisho ya imani. Wanglikana huvisoma kwa ajili ya maarifa tu, na siyo kwa mafundisho ya imani. Tunaamini kwamba vitabu hivi vinavutia, vina ujuzi na vyafaa kusomwa.

**10. Amua Kusoma *The Message or the Story*, yaani 'Ujumbe' au 'Masimulizi' –** *the Message,* yaani kitabu cha 'Ujumbe' ni ufupisho wa biblia uliyoandikwa na Eugene Petersen, mchungaji na mwandishi wa vitabu vya kiroho, ambao unafanya masimulizi ya Biblia na vifungu vyake kuleta maana zaidi, katika njia mpya. Tembelea tovuti hii:www.messagebible.com *The Story*, yaani kitabu cha 'Masimulizi' kimechapishwa na Zondervan, ni mkusanyiko wenye mfululizo wa masimulizi ya Biblia yaliyosukwa katika simulizi moja lisilokatika kama vile usomavyo kitabu cha hadithi. Masimulizi yameunganishwa na paragrafu maalumu zinazoelekeza jambo linalofuata. Maelezo marefu ya kanuni za vyakula, maelezo ya nasaba na masimulizi yanayojirudiarudia yahusuyo wafalme wa kale yameondolewa kabisa. Tembelea tovuti hii: www.thestory.com Kitabu cha *The Message, 'Ujumbe' na kile cha The Story, 'Masimulizi'* ni vya msaada sana na vinavutia kwa watu ambao wamesumbuka namna ya kusoma Biblia.

**11. Soma Bibli katika lugha tofauti –** Jikumbushe lugha yako ya Kihispania, Kilatini au Kifaransa na usome Biblia kwa lugha ya kigeni. Utajijengea upya ujuzi wako wa lugha, na lililo la muhimu zaidi ni kwamba masimulizi ya Biblia uliyoyazoea utayaelewa kwa upya kwa njia mpya utakaposoma kwa lugha ya kigeni. Kwa wasomaji wa Kifaransa tunawashauri wasome *La Nouvelle Bible de Jerusalem*, wasomaji wa Kihispania wasome *Santa Biblia Dios Habla Hoy* ambalo ni toleo la *American Bible Society,* yaani Chama cha Biblia cha Marekani; na kwa wasomaji wa Kilatini wasome Biblia ya Kilatini iitwayo *La Vulgata*.

**12. Soma kitabu cha Biblia ukiwa na kitabu cha Mafafanuzi –** Anza kwa kusoma mojawapo ya injili. Kisha endelea na Kitabu cha Matendo, baadhi ya nyaraka za Paulo na vitabu vya Agano la Kale kama vile Mwanzo, Kutoka, I na II Samweli, Isaya, Yeremia na Zaburi. Unaweza kufanya hivyo ukiwa peke yako au katika kikundi na wengine. Tafuta kitabu cha Timothy Johnson kiitwacho *The Writings of the New Testament*, yaani 'Maandiko ya Agano Jipya' ni utangulizi mzuri sana ukiwa na sura moja ikielezea kitabu kimoja katika Agano Jipya. Tunashauri pia upate mfululizo wa Mafafanuzi uliyo yafuatayo: 1) *The People's Bible Commentary Series,* yaani 'Mfululizo wa Mafafanuzi ya

Biblia ya Watu' unaochapishwa Uingereza na 'Umoja wa Kujisomea Biblia' uitwao kwa Kiingereza *Bible Reading Fellowship*; mfululizo huo umetolewa na waandishi na wanazuoni mahiri akiwemo Profesa Richard Burridge; Tembelea tovuti hii: www.brfonline.org.uk 2) *The New Daily Bible Study Series,* yaani 'Mfululizo wa Mtaala Mpya wa Biblia wa Kila Siku', unaosambazwa na Westminster John Knox Press na umeandikwa na William Barclay, ni ufafanuzi mzuri na mwepesi kusoma na umejaa mifano hai. Tembelea tovuti hii: www.wjkbooks.com 3) *The For Everyone Bible Study Guides,* yaani 'Muongozo wa Mtaala kwa Kila Mmoja', umechapishwa na chama kiitwacho *the Society for Promoting Christian Knowledge in England,* yaani 'Chama cha Uenezaji wa Maarifa ya Kikristo nchini Uingereza' na muongozo huo umeandikwa na Tom Wright. Tembelea tovuti ya: www.amazon.com na 4) *The Old Testament New Daily Bible Study*, yaani 'Mtaala wa Biblia wa Kila Siku wa Agano la Kale', uliochapishwa na *Westminster John Knox Press* na kuandikwa na John L. Gibson. Tembelea tovuti ya: www.wjkbooks.com

**13. Soma maandiko mengine mazuri ili yakusaidie unaposoma Biblia** – Pitia toleo la Mtaala wa Biblia katika Maisha ya Kanisa, pia andiko la *Deep Engagement Fresh Discovery*, yaani 'Kukutana na Ugunduzi Mpya na Kina', linalopatikana kupitia tovuti ya Jumuiya ya Kanisa Anglikana duniani: www.anglicancommunion.org Pia tunapendekeza mfululizo uliochapishwa na Morehouse Publishing uitwao *Conversations with Scripture*, yaani 'Kuzungumza na Maandiko', ulioandaliwa kwa ushirikiano na *Anglican Association of Biblical Scholars*, Ushirikika wa Kianglikana wa Wataalam wa Biblia. Katika wale waliochangia makala wamo Marcus Borg, Cynthia Kittredge, Stephen Cook na wengine. Kwa wale ambao wangependa kuzama zaidi katika kujifunza Biblia, tunapendekeza kitabu cha Bruce Metzger kiitwacho *Oxford Companion to the Bible*, yaani 'Msaada wa Biblia wa Oxford', ni hazina nzuri ndani ya toleo moja na inayoweza kusomeka vizuri.  Pia tembelea tovuti hii: www.thecenterforbiblicalstudies.org na uangalie mahali palipoandikwa "Resources" pakiwa na maana ya 'maandiko' ili upate orodha ya vitabu vihusuvyo Biblia ambavyo tunashauri uvisome.

**14. Jifunze Kusoma Biblia katika Lugha zake za asili** – Jaribu kusoma Kiebrania cha Kibiblia kwa mwalimu wa kiebrania (rabi) aliye karibu nawe, au jifunze Kiyunani (Kigiriki cha zamani) ili uweze kuelewa mambo mapya unaposoma Biblia katika lugha yake ya asili.  Zipo tovuti zinazoweza kukuwezesha kufanya hivyo.  Hazina moja inayoweza kukupa mwanga zaidi ni tovuti ya www.interlinearbible.org, ambayo inakupa toleo lililotoholewa la Agano Jipya la Kiyunani na Agano la Kale la Kiebrania, na linakuunganisha na maana ya kila neon la Kiyunani na Kiebrania katika Biblia. Tovuti nyingine kama YouVersion.com zinakupa Biblia katika lugha nyingine zaidi, licha ya matoleo mengi ya Kiingereza.  Tafsiri za Kijerumani, Kikorea, Kiswahili na Kiswideni zinaweza kusomwa sambamba na zile za Kiingereza ambazo utakuwa umechagua.

**15. Tembelea Nchi Takatifu** – Nchi Takatifu hutolewa kama injili ya tano. Hakuna cha kufananisha kama kwenda katika Nchi Takatifu na kukanyaga kwenye nyayo za Yesu na watu wakuu wa Biblia. Makundi mengi huandaa utaratibu wa safari nzuri za kwenda katika Nchi Takatifu. Tunawendekeza shirika la *Worldwide Pilgrimage*, yaani 'Hija ya Ulimwengu Pote'. Tembelea tovuti yao ya:www.worldwidepilgrimage.com

## Maoni kwa Washiriki wa vikundi vidogo vya Biblia

**1. Jiunge au anzisha Mtaala wa Biblia –** Biblia hueleweka vyema zaidi tunapoisoma tukiwa na wengine. Kwa kadri tunavyosoma Maandiko pamoja, tunajifunza kwa wenzetu pia. Kiini cha imani siyo kuwa na majibu yote bali kuuliza majibu sahihi. Mitaala ya Biblia inatusaidia kuwa na majibu sahihi. Muulize mchungaji au kiongozi wako wa kanisa kuhusiana na mtaala wa Biblia unaokufaa. Unaweza kuanzisha mtaala wa Biblia nyumbani kwako, shuleni au kanisani. Waalike marafiki, familia na waumini wa kanisa lako, Klabu ya kujisomea vitabu, majirani na wafanyakazi wenzako ili wajiunge nawe. Chagua kitabu cha Biblia na mjifunze kwa uangalifu. Tunashauri uanze na injili au usome Injili ya Luka na kisha usome Kitabu cha Matendo. Kisha amua kusoma nyaraka za Paulo kwa Warumi au Waraka wa kwanza na wa pili wa Wakorintho. Kama ukiamua kusoma Agano la Kale, tunapendekeza uanze na Mwanzo na Kutoka. Vitabu hivi vyenye kuvutia husaidia kufunua historia ya wokovu, Agano na mpango wa Mungu kwa wanadamu.

**2. Education for Ministry (EfM), yaani 'Elimu ya Huduma Takatifu (EyHT)'** – Mpango huu, ulioanzishwa na Chuo Kikuu cha Sewanee ya Kusini, huko Tennessee, ni wa miaka mine ambao huanza shabaha ya kina ya kujifunza Agano la Kale kwa mwaka mmoja ukifuatiwa na mafunzo ya Agano Jipya ya mwaka mmoja. Katika mwaka wa tatu washiriki hulenga zaidi Historia ya Kanisa. Mwaka wa nne hutengea kwa ajili ya mafunzo ya theologia. EfM ni hatua nzuri kwa watu ambao wameshashiriki Changamoto ya Biblia na wana maswali mengi yasiyo na majibu. Washiriki hujiandikisha kwenye mpango huu kwa mwaka mmoja mmoja.

EfM huhusisha kwa kiasi kikubwa usoma wa Biblia, mazoezi baada ya darasa na majadiliano ya vikundi. Kila kikundi cha EfM huongozwa na msimamizi aliyefunzwa vyema. EfM yawezekana ndiyo mpango wa juu kabisa wa elimu unaotolewa na Kanisa la Marekani. Umepangiliwa vizuri na huwasaidia washiriki kuelema mambo makuu ya Biblia, na kuyatumia mafunzo ya Biblia katika maisha yao na kuyadhihirisha katika safari ya maisha yao ya kiroho. Kwa watu wengi, mpango wa EfM ni uzoefu unaobadilisha maisha yao. Ili kujifunza zaidi, wasiliana na mchungaji wako au tembelea tovuti hii: www.sewanee.edu/EFM/ au www.edowefm.org

**3. Shiriki katika Mpango wa *the Disciples of Christ in Community (DOCC)*, yaani 'Wafuasi wa Kristo katika Jamii (WKKJ)' –** mango huu unatafuta kuimarisha kila

kanisa kwa kuwasaidia waumini kupokea na kutoa upendo wa Kristo.  Ulianza takribani miaka 40 iliyopita katika Kanisa la Trinity Episcopal la New Orleans, mpango huu wa DOCC umeshapata wahitimu 35,000 walioshiriki kutoka katika makanisa zaidi ya 400. Kila juma, kwa kipindi cha zaidi ya miezi mitatu au minne, wachungaji au walei waliofunzwa hutoa mafundisho ya dakika 40 yanayogusa kiini cha imani, yakijengwa kwenye msingi wa Maandiko.  Viongozi wa vikundi vidogo waliofuzu mafundisho huwasaidia washiriki kujifunza pamoja kwa kadri wanavyoyatumia mambo makuu ya imani ya Kikristo katika maisha yao. Kila kikundi kidogo hujitahidi kuwa 'jamii ndogo yenye upendo.' Tabia hiyo ya upendo husambaa katika kanisa zima.  Unahitaji kutumia masaa kumi na nane ya kuwafunza watoa mada na viongozi wa vikundi vidogo.  Ili kujifunza zaidi, wasiliana na mchungaji wa mtaa wako au Mch. Canon William Barnwell kwa anuani hii wbarnwell@trinitynola.com au tembela tovuti hii ya: www.natonalcathedral.org/learn/docc.shtml au www.trinitynola.com/DOCC

**4. Shiriki katika mpango wa *Transforming Literature of the Bible* (TLB), yaani 'Maandiko ya Biblia yenye Mabadiliko (MBM)' –** Kozi ya juma 36 ya Maandiko ya Biblia yenye Mabadiliko hujitahidi kuhusianisha mafundisho makuu ya Biblia na mambo ya maisha yetu ya kila siku. Wanafunzi wanapokuwa wamesoma Biblia kwa mwaka mmoja kupitia mpango wa *The Bible Challenge,* Changamoto ya Biblia, wanaweza kujaribu kozi ya TLB. Washiriki wa kozi huchimba ndani zaidi katika vifungu na masimulizi ya Biblia yaletayo mabadiliko kutoka Mwanzo, Marko na Warumi.  Katika mtindo wa semina, washiriki hutafakari vifungu na kutumia ipasavyo vitabu vya mafafanuzi.  Kwa kutumia maswali yaliyopendekezwa, huhusianisha vifungu vya Biblia na maisha yao wenyewe.  Unahitaji masaa nane hadi kumi ya kuwafundisha mahali pamoja viongozi wa semina na washiriki. Wachungaji na walei wenye uzoefu huongoza mafunzo hayo. Ili kujua zaidi, wasiliana na mchungaji wako au Mch. Canon William Barnwell kwa anuani hii ya barua-pepe wbarnwell@trinitynola.com.

**5. Shiriki kwenye Mtaala wa Biblia wa 'Kerygma', yaani 'Uenezi'** – maandiko yaliyoandaliwa ya mpango wa Kerygma yanasisimua na kutoa changamoto kiakili na kiroho. Viongozi wa Kerygma hupewa mafunzo na kupata kitabu cha muongozo ambayo kimetengenezwa mahsusi kutoa fursa zinazoamsha majadiliano na kuleta ufahamu zaidi wa maandiko ya Biblia kupitia mikutano ya vikundi vidogo. Kwa taarifa zaidi, tembelea tovuti hii ya www.kerygma.com

Ikiwa Changamoto ya Biblia imekuletea uzoefu mzuri wa kiroho na imegusa moyo wako na kukuletea baraka nafsini mwako, nakualika uchangie Kituo cha Masomo ya Biblia ili kusaidia kukuza Changamoto ya Biblia ulimwenguni mote ili wengine wanufaike na usomaji wa Neno la Mungu kila siku na kushiriki katika Changamoto ya Biblia.  Sadaka yako inaweza kutolewa kwa "*Christ Church Greenwich*" ukieleza ni kwa ajili ya "*The CBS*" na uitume kwenda Christ Church Greenwich 254 E. Putnam Avenue, Greenwich, CT 06830.

Mungu na akubariki kwa wingi wa utajiri wake unapojifunza Maandiko, nuru na upendo wa Mungu vikubadilishe maisha yako na kukuangazia kila siku.

Ili kujiunga na Changamoto ya Biblia, tafadhari tuma barua-pepe kwa anuani hii: mzabriskie@christchurchgreenwich.org.

Mch. Marek P. Zabriskie

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Christ Church Greenwich (Connecticut), na Mwanzilishi wa Kituo cha Masomo ya Biblia na Changamoto ya Biblia.

©

St. Thomas' Church
WHITEMARSH
*Come with us on a journey with Christ*

Bethlehem Pike and Camp Hill Road
Fort Washington, PA 19034
215-233-3970
*stthomaswhitemarsh.org*